WATOTO KWANZA

IMPROVING ACCESS TO AND QUALITY OF EARLY CHILDHOOD EDUCATION IN ZANZIBAR

FINAL EVALUATION

EXECUTIVE SUMMARY / DIBAJI

KISWAHILI

دبي العطاء
Dubai Cares

SAMUEL HALL.

Samuel Hall conducted the final evaluation of Watoto Kwanza.

Dubai Cares funded Watoto Kwanza over a period of four years (2014-2017).

The **Aga Khan Foundation** (AKF) was the grant manager for Watoto Kwanza.

The **Madrasa Early Childhood Programme – Zanzibar** (MECP-Z) was the main implementing partner for Watoto Kwanza.

The **Ministry of Education and Vocational Training** (MoEVT) was the public implementing partner for Watoto Kwanza.

This publication was commissioned by Dubai Cares. It was prepared and conducted by Samuel Hall. The views and analysis contained in the publication therefore do not necessarily represent the views of Dubai Cares. Any errors are our own and should not tarnish the reputations of others.

This document should be cited using the following referencing style:
Samuel Hall (2018). *Watoto Kwanza: Improving access to and quality of early childhood education in Zanzibar – Final Evaluation, Executive Summary (English)*, commissioned by Dubai Cares.

Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya gharama nafuu au visivyo na gharama kabisa, katika shule ya jamii ilioko Unguja (Magharibi)

Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya gharama nafuu au visivyo na gharama kabisa, katika shule ya serikali ilioko Pemba (Micheweni)

ORODHA YA AKRONIMU

AKF	Aga Khan Foundation
MECP-Z	Programu ya Makuzi na Maendeleo ya watoto, Zanzibar
WEMA	Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali

DIBAJI

Umuhimu wa Elimu ya Maandalizi umekuwa ukipata kipaumbele katika miaka ya karibuni. Malengo Endelevu ya dunia ya mwaka 2015 yameweka kuwa, ifikapo mwaka 2030, "makuzi na upatikanaji wa elimu bora ya maandalizi kwa watoto wote" ni lengo maalum. Hapa Zanzibar, lengo hili limekuwa likipewa kipaumbele kwa kadiri siku zinavyokwenda. Serikai kupitia sera yake ya Elimu ya mwaka 2006, imeifanya elimu ya maandalizi kuwa sehemu ya elimu ya lazima kwa wototo wote. Kama hayo hayatoshi, taasisi zisizo za kiserikali zimekuwa zikitoa mchango mkubwa katika utoaji wa elimu ya maandalizi au huduma za makuzi na maendeleo ya watoto (maneno yote mawili yanatumika sawa katika ripoti hii).

Utafiti huu umeangalia juu ya utekelezaji wa mradi wa "*Watoto Kwanza*" na namna ulivyozikabili changamoto mbalimbali zinazoikumba sekta ya elimu ya maandalizi hapa Zanzibar, kimkabala na kiufanisi, na kwa kiasi gani sekta hii imeweza kuwa endelevu kuanzia mwaka 2013. Mradi huu ulitekelezwa kwa pamoja chini ya ufadhili wa Dubai Cares, Aga Khan Foundation (AKF), Programu ya Makuzi na Maendeleo ya watoto, Zanzibar (MECP-Z) na Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali (WEMA), katika visiwa vya Unguja na Pemba, kuanzia mwaka 2014 hadi 2017. Mbali ya kuutathmini mradi huu katika maeneo yake makuu matatu; mafunzo kwa walimu, ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia, na uboreshaji wa mfumo wa utowaji elimu na mahusiano ya kiutendaji baina ya maskuli, utafiti huu pia umeangalia juu ya mwenendo na mafanikio yaliyopatikana katika mazingira ya sasa ya utoaji wa elimu ya maandalizi. Mwisho kabisa, ripoti hii inatoa mapendekezo kadhaa kulingana na mambo yaliyobainika kupitia utafiti huu katika ngazi tatu: mapendekezo mahsusi kwa mradi wa *Watoto Kwanza*, mapendekezo mahsusi kwa sekta nzima ya elimu ya maandalizi na pia inatoa mapendekezo ya kiujumla kwa sekta nzima ya elimu hapa Zanzibar.

Samuel Hall (Watafiti) wametumia mbinu mbalimbali ikiwemo madodoso yaliyokusanya taarifa zinazoonyesha ubora na idadi, ili kuweza kukusanya taarifa za kutosha juu ya mradi huu na matokeo yake ndani ya kipindi cha mwezi mmoja (Februari-Machi 2018) katika wilaya nane za Unguja na Pemba. Taarifa katika ripoti hii zinajumuisha mapitio ya nyaraka mbalimbali, mahojiano ya watu zaidi ya 30, majadiliano ya watu mbalimbali yaliyovishirikisha vikundi 20, uchunguzi wa moja kwa moja katika madarasa 51, na mahojiano ya moja kwa moja na zaidi ya walimu 500 waliohusika katika mradi wa *Watoto Kwanza*. Zaidi ya hayo, warsha ya washikadau mbalimbali ilifanyika ndani ya mwezi wa Mei 2018, ili kuichangia ripoti hii na mapendekezo yake.

TATHMINI YA MRADI WA *WATOTO KWANZA* NA MAENEO YAKE MATATU MUHIMU:

Kupitia mbinu mbalimbali zilizotumika, utafiti huu unatoa picha nzuri juu ya mafaniko ya mradi na namna mafanikio hayo yalivyofikiwa. Mradi wa *Watoto Kwanza* ulibuniwa na kutekelezwa huku ukizingatia kwa kiasi kikubwa uhalisia, uwezo wake wa kufikia malengo yaliyopangwa na namna ambavyo unajitosheleza. Hata hivyo, suala la uendelevu wa mradi huu linatia wasiwasi mkubwa.

Kwa upande wa uendelezaji wa walimu kitaaluma, tatizo kubwa lililokuwepo la kujenga utaalamu wa walimu katika sekta ya makuzi na maendeleo ya watoto limeshughulikiwa ipasavyo kuanzia kipindi mradi ulipobuniwa mwaka 2013/2014, hadi katika utekelezwaji wake. Baadhi ya mafanikio na changamoto ni:

+ Mafunzo yenye ubora wa hali ya juu yametolewa kwa walimu 896 wa kozi mbili tofauti, wakiwemo wale walioko kazini na wale ambao hawajaajiriwa. Mafunzo yote haya yalitayarishwa na kutolewa kwa mashirikiano ya pamoja na WEMA, sio tu yalipelekea kutambuliwa rasmi kwa walimu hao na serikali, bali pia kuandaliwa kwa mtaala wa pamoja wa ngazi ya maandalizi kwa matumizi ya baadaye.
+ Walimu walionyesha kuridhishwa kwao na mafunzo walioyapata na athari za mafunzo hayo katika maisha yao kwa ujumla (hali hii ilijitokeza kwa walimu zaidi ya asilimia 98).
+ Utekelezaji wa mradi ulizingatia sana namna ya kubadilisha ufundishaji kwa mazoea. Kwa mfano, mfumo wa usaidizi wa wakufunzi kwa kusomesha kwa pamoja na walimu wao (ambao walimu waliupenda sana) ulitiliwa mkazo sana wakati wote wa utekelezaji wa mradi
- Tatizo kubwa katika kipengele hiki ni kukosekana kwa ajira rasmi kwa walimu ambao hawajaajiriwa na ambao tayari wameshapata mafunzo ya ualimu katika ngazi hii. Ingawa mradi ulifanya kazi kubwa ya kujenga uwezo wa walimu kwa kuongeza idadi ya walimu wenye sifa za kufundisha katika ngazi hii, kuna changamoto ya ukosefu wa ajira rasmi kwa wale ambao bado hawajaajiriwa. Ni moja tu kati ya robo tatu ya walimu waliokwishapata mafunzo, ndio ambao hadi sasa wamefanikiwa kupata ajira (kwa wale waliopata mafunzo kabla ya kuajiriwa - idadi ya waliopata ajira inashuka hadi asilimia 10). Badala yake, karibu nusu nzima ya walimu waliopata mafunzo chini ya mradi huu wameamua kuendelea kufundisha kwa njia ya kujitolea (bila mshahara), jambo ambalo ni kama vile njia ya kujiweka tu ndani ya fani hii na huku wakisubiri kama itatokezea nafasi ya kuajiriwa kama walimu rasmi. Bila ya kuchukuliwa hatua madhubuti, mafanikio haya mazuri yaliyokwisha patikana chini ya mradi huu, mustakbali mzima wa elimu ya maandalizi utakuwa mashakani, kwani walimu hawa wanaojitolea tayari wameanza kuchoka na kazi hii kutokana na kuvunjika moyo, jambo ambalo litawapelekea watu kuiona fani hii kuwa si kazi ya kutegemea.

Tathmini juu ya mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia: Suala hili, licha ya kupata mafanikio na kupendwa sana na walimu, utekelezwaji wake umekuwa hauridhishi.

+ Walimu 533 walipatiwa mafunzo ya siku tatu juu ya utengenezaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya gharama nafuu au visivyo na gharama kabisa. Mafunzo haya yaliwavutia sana walimu kwani yalitoa matokeo mazuri na yanayoonekana katika skuli nyingi za hapa Zanzibar.
- Mradi wa *Watoto Kwanza* ulijumuisha pia kipengele cha kuzipatia skuli vifaa (kama vile vitabu, mageleni ya kuhifadhia vitu, mabusati, na kadhalika). Wakati skuli 316 zilipatiwa vifaa hivi, utafiti huu umegundua kuwa upatikanaji wa vifaa hivi haukuwa na uwiano hasa kwa kuzingatia idadi ya vifaa vilivyotolewa na umadhubuti wake. Kinadharia, ingawa mafunzo ya utengenezaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia yaliweza kukidhi changamoto ya ukosefu wa vifaa kwa skuli za maandalizi za Zanzibar, utekelezaji wake umeonyesha kasoro kubwa hasa ukizingatia utoshelevu, umadhubuti na kudumu kwa vifaa vyenyewe, ikilinganishwa na matakwa ya mafunzo ya utengenezaji wa vifaa.

Uimarishaji wa mifumo na mashirikiano: Chini ya kipengele hiki, kulianzishwa na kuimarishwa mfumo wa uendeshaji wa skuli kwa mashirikiano ya kikanda (klasta). Hata hivyo, athari ya moja kwa moja juu ya mwamko na ushiriki wa jamii ambao unaweza kunasibishwa na mradi wa *Watoto Kwanza* ni mdogo sana.

+ Mfumo wa uimarishaji wa uendeshaji skuli kikanda (klasta) unaendelea huku asilimia 75 ya walimu wakionyesha kuwa skuli zao ziko chini ya mfumo huu, ambapo vikao vinavyojadili masuala muhimu ya maendeleo ya sekta ya elimu ya maandalizi vinafanyika kikawaida. Zaidi ya hayo, suala zima la uratibu wa mfumo huu (klasta), limeachiwa chini ya WEMA na Maafisa Elimu wa Wilaya.

- Utafiti huu unaonyesha kuwa ushirikishwaji wa jamii na wazazi katika mradi wa *Watoto Kwanza* ulikuwa mdogo, kwani ilitarajiwa kuwa vikundi vidogo vidogo vya wazazi na jamii vilitarajiwa kwanza kuufahamu mradi wao wenyewe na baadaye wawaelezee wenzao kuhusu mikakati ya mradi huu. Ni wachache tu kati yao ndio walioonyesha angalau kuwahi kusikia kuhusu mradi huu. Badala yake, serikali ndio inayoonekana kuwa kinara wa sekta nzima ya makuzi na maendeleo ya watoto. Kukosekana huku kwa uelewa na ushirikishwaji finyu wa jamii, kunaweza kuwa kikwazo kikubwa juu ya umiliki na ushiriki wa jamii katika sekta hii.

NAFASI YA MRADI WA *WATOTO KWANZA* KATIKA MAGEUZI YA SEKTA YA MAKUZI NA MAENDELEO YA WATOTO

Mradi wa *Watoto Kwanza* ulilazimika kuangalia kwa makini changamoto za kimazingira na kimfumo zinazoweza kuathiri utekelezaji wa mradi na kufikia malengo yake:

- Katika siku za karibuni, huduma ya elimu ya maandalizi imekuwa ikipitia katika mabadiliko muhimu (kuongezeka kwa juhudi za serikali katika usimamizi na kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa watoto katika ngazi ya maandalizi).
- Kasoro mbalimbali (kama vile uwiano mkubwa wa wanafunzi kwa mwalimu, na uhaba mkubwa wa madarasa). Mradi wa *Watoto Kwanza* ulikuwa ni hatua njema ya kuelekea kuzuri, ingawa uliweza kushughulikia vizuri moja tu kati ya matatizo mengi yanayoikabili sekta hii.
- Hata hivyo, ukosefu wa mikakati madhubuti pamoja na uwekezaji finyu wa fedha za kutosha kwenye sekta hii, unarudisha nyuma mafanikio yaliyokwishapatikana, kama vile mafanikio yaliyotokana na mradi wa *Watoto Kwanza*.

Mradi huu umeweza kuboresha mfumo mzima wa utoaji elimu ya maandalizi (kwa mfano: mfumo wa uendeshaji wa maskuli kupitia mashirikiano ya kikanda (klasta), utumiaji wa mtaala uliotatayarishwa kwa pamoja kati ya WEMA na MECP-Z. Hata hivyo, kimtazamo, kunaonekana kuwepo kwa fursa inayoelekea kupotea, ambayo ingeweza kusukuma mbele maendeleo ya sekta hii pamoja na kudumisha mafanikio yaliyokwishapatikana chini ya mradi wa *Watoto Kwanza*. Miongoni mwa fursa hizo ni kukosekana kwa juhudi madhubuti za kuwaajiri walimu waliokwishapata mafunzo ya ualimu katika ngazi ya maandalizi, utekelezaji hafifu wa mafunzo yaliyokwishapatikana juu ya utayarishaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutokuwashirikisha wazazi katika kuchangia huduma za uendeshaji wa elimu hii (kwa mfano, kulipia angalau posho za walimu wanaojitolea). Juhudi zaidi zinahitajika ili kuboresha mfumo mzima wa sekta hii. Ushiriki wa jamii na kuwajengea uelewa mzuri kwamba miradi kama hii, ni juhudi za uanzishaji na za muda tuu, vinahitajika kuzingatiwa sana katika miradi mingine ijayo.

Tukiangalia mbele, mbali ya tatizo kubwa la ufinyu wa bajeti kama ilivyoelezwa hapo awali, ukosefu mkubwa wa miundo mbinu mwafaka unatoa changamoto kubwa katika sekta ya elimu ya maandalizi hapa Zanzibar. Bila ya madarasa mazuri na ya kutosha, ushiriki na ufanisi wa watoto katika skuli hizi utakuwa mashakani. Wasiwasi huu ni wa wazi hasa ukizingatia ongezeko kubwa la uandikishaji wa watoto katika ngazi hii hapa Zanzibar. Vikwazo vingine kwa upande wa wazazi vinaendelea kuwa ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununulia sare za skuli na malipo ya usafiri kwa watoto wao, ukosefu wa mwamko wa kutosha miongoni mwa wazazi juu ya umuhimu wa elimu ya maandalizi kwa mtoto, na kutokuwa na uhakika wa usalama wa watoto wakati wanapokwenda na kurudi skuli (katika maeneo yaliyo mbali na skuli). Zaidi ya yote hayo, mabadiliko

ya kimfumo yanayotokea hivi sasa kama vile ugatuzi (madaraka mikoani) na mabadiliko ya mtaala wa maandalizi yanahitaji kuzingatiwa kwa makini katika mipango na programu zitakazokuja baadaye.

MAPENDEKEZO

Mbali ya kufanya tathmini ya mradi wa *Watoto Kwanza*, ripoti hii pia imekusudia kutoa mapendekezo ambayo yatapelekea upatikanaji wa huduma bora za malezi na makuzi ya watoto hapa Zanzibar. Kwa mnasaba huo basi, ripoti hii inatoa mapendekezo yake katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo:

1. **Mapendekezo mahsusi yatakayoboresha mafanikio yaliyokwishapatikana katika mradi wa *Watoto Kwanza*:**
    1. Kutilia mkazo suala la kuwaajiri walimu waliokwishapata mafunzo ya ualimu kwa ngazi ya maandalizi
    2. Kuendeleza juhudi zilizokwisha fanyika katika kuboresha mtaala na nguvu kazi iliyokwisha jengeka
    3. Kuulea na kuuboresha mfumo wa mashirikiano ya skuli kikanda (klasta) kwa skuli ambao tayari umekwisha jengwa

2. **Mapendekezo ya kijumla kuhusu sera na mipango ya elimu ya maandalizi:**
    1. Kuratibu ushiriki wa washikadau wote katika kuandaa mipango ya sekta hii
    2. Kuhakikisha kuwepo kwa mipango mizuri ya baadaye pamoja na mfumo mzuri wa ufuatiliaji na tathmini

3. **Mapendekezo mahsusi juu ya kuzikabili changamoto zilizoainishwa juu:**
    1. Kuufanyia mapitio Mtaala wa Elimu ya Maandalizi
    2. Kufanyia mapitio sera na taratibu, na baadaye kuzifuata katika uajiri wa walimu
    3. Kukuza mwamko wa wazazi na jamii juu ya umuhimu wa kuwaandikisha watoto wao katika elimu ya maandalizi na ushiriki wao kwa ujumla
    4. Kubuni na kujenga majengo na miundo mwafaka kwa watoto wadogo

Kutokana na uzoefu, utaalamu, na mamlaka yao, watekelezaji wakuu wa mradi wa *Watoto Kwanza* – AKF, MECP-Z na WEMA – wana nafasi nzuri ya kuipeleka mbele sekta ya Elimu ya Maandalizi, ili iwe bora na endelevu hapa Zanzibar.

Vifaa vya michezo katika shule ya serikali ilioko Unguja (Magharibi)

SAMUEL HALL.

Samuel Hall is a social enterprise dedicated to research in countries affected by migration. Our mandate is to produce research that delivers a contribution to knowledge with an impact on policies, programmes and people.

Samuel Hall has offices in Afghanistan and Kenya, and a presence in Germany, Senegal, and Ethiopia. For more information, please visit **www.samuelhall.org**